

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA TISA

18 APRILI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA TISA – TAREHE 18 APRILI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

108. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Wahitimu wangapi wa Vyuo wanafanya kazi ya kujitolea na wangapi wameajiriwa na kujiajiri baada ya kujitolea.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

109. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Hosteli za Wanafunzi katika Shule zilizopo pembezoni mwa Mkoa wa Katavi.

110. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI (MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatenga fedha kumaliza Bweni la Wasichana Shule ya Sekondari Jana katika Halmashauri ya Msalala.

111. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza Madaktari Bingwa na Wauguzi katika Vituo vya Afya Mkalama.

112. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini majengo ya zamani ya Halmashauri ya Bunda DC yasitumike kuwahudumia Wananchi wa Jimbo la Bunda.

WIZARA YA UJENZI:

113. MHESHIMIWA SAMWELI XADAY HHAYUMA (HANANG’):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Nangwa – Gisambalang hadi Kondoza kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA MAJI:

114. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga mradi wa maji Lutale Langi kwa kuwa usanifu umekamilika.

WIZARA YA FEDHA:

115. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali inatambua athari hasi kwa Jamii ya Watanzania zinazotokana na ongezeko kubwa la michezo ya kubahatisha.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

116. MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI (CHEMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga mnara wa Mawasiliano katika Kata ya Kimaha Kijiji cha Mwaikisabi – Chemba.

117. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMEDI KUCHAUKA (LIWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya maboresho ya minara iliyojengwa na Halotel Liwale ili iweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
18 APRILI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**